# JARIDA LA MAFANIKIO- SONGEA MC



MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN
RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## TATHIMINI YA MAFANIKIO YA MIAKA 5 CHINI YA UONGOZI WA DKT. SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.



DKT. DAMAS NDUMBARO (MB)
WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA

**KUANZIA 2020 HADI 2025**

# YALIYOMO

1. Utangulizi.
2. Utekelezaji Sekta ya Elimu.
3. Taarifa za Miradi Sekta ya  Afya.
4. Hali ya Utoaji wa  Mikopo ya Asilimia 10%
5. Utoaji na Matumizi ya Pembejeo za Ruzuku  kwa Wakulima.
6. Picha za Matukio Mbalimbali za Miradi ya Maendeleo.
7. Mwisho

# UTANGULIZI

*Tunaishukuru Serikali ya awamu ya sita chini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan , Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuboresha huduma na miundombinu mbalimbali ya miradi ya maendeleo yenye thamani ya Bil. 188.*

*Katika kipindi cha miaka (5) 2020-2025 Manispaa ya songea imejenga jumla ya madarasa 244, vituo vya afya zaidi ya 6, Hospitali ya Manispaa 1, Zahanati zaidi ya 4, Barabara, Mikopo kwa vikundi ya 10% zaidi ya Bil. 2 zimetolewa pamoja na huduma mbalimbali za kijamii.*

*KAZI NA UTU; Tunasonga mbeleee……*

## Mafanikio ya Halmashauri ya Manispaa ya Songea (Miaka 5 ya Utekelezaji):

### Takwimu Muhimu za Kiutawala

**Idadi ya Tarafa:** 2
**Idadi ya Kata:** 21
**Idadi ya Mitaa:** 94
**Jimbo la Uchaguzi:** 1

# SEKTA YA ELIMU

Jumla ya Madarasa Mapya: 244
- Thamani: Tsh. 5.234 Bilioni (pamoja na madawati, meza, viti)

Shule Mpya za Sekondari: 4
- Dr. Lawrance Gama, Luhira, Dr. Damas Ndumbaro, Amali Ruvuma (maalum)
- Thamani ya ujenzi: Tsh. 3.6 Bilioni

Shule Maalumu ya Awali na Msingi (Kiingereza):
- Gharama: Tsh. Mil. 800 (mapato ya ndani)
- Wanafunzi: 491

Fedha za Elimu Bure (kwa mwezi): Tsh. Mil. 298
- Sekondari: Tsh. Mil. 231
- Msingi: Tsh. Mil. 67

Jumla ya fedha kwa Elimu katika kipindi hiki: Tsh. 14.24 Bilioni

Chuo Kikuu cha Uhasibu (Pambazuko):
- Gharama: Tsh. 17.8 Bilioni
- Jumla ya fedha sekta nzima ya elimu (pamoja na fidia): Tsh. 41.78 Bilioni

## SEKTA YA AFYA

Jumla ya Fedha: Tsh. 6.735 Bilioni

- Hospitali ya Manispaa: 1
- Vituo vya Afya: 4
- Zahanati: 4

- Fedha za Matibabu (kwa mwezi): Tsh. 40.7 Milioni
  - Awali: Tsh. Mil. 18 tu

## SEKTA YA HUDUMA ZA KIUCHUMI

TASAF: Tsh. 9 Bilioni kwa walengwa 2,514

Ruzuku ya Mbolea:

Wakazi Waliofaidika: 60%

Mbolea Iliyotolewa: Tani 88,208

## Fidia ya Maeneo ya Maendeleo:

- EPZA Mwenge Mshindo: Tsh. 5.3 Bilioni
- Bonde la Ruhira: Tsh. Bil 1.9
- Sambamba na Utwaaji wa maeneo na utatuzi wa changamoto.

## Mikopo kwa Makundi Maalumu:

- Wanawake (4%), Vijana (4%), Watu wenye Ulemavu (2%)
  - Jumla ya Mikopo: Tsh. 2.205 Bilioni
  - Mikopo inayotarajiwa kupitia NMB: Tsh. 1.3 Bilioni

**Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani:**

- Zamani: Tsh. 2.1 Bilioni
- Sasa: Tsh. **7.2 Bilioni**
- Matarajio ya Bajeti ya 2025/2026: Tsh. 9.1 Bilioni

**Hitimisho:**

Dkt. Ndumbaro ameonyesha utekelezaji mzuri wa miradi ya maendeleo, kwa ushirikiano na Serikali Kuu. Miradi hiyo inaonekana kuboresha maisha ya wananchi kwa kiwango kikubwa katika elimu, afya, huduma za jamii, kilimo na uchumi wa ndani.

Elimu ya msingi na sekondari

Huduma za afya kwa wananchi

Miundombinu ya kijamii

Uwezeshaji wa makundi maalumu

Kilimo na ustawi wa kaya

Mafanikio haya yanadhihirisha dhamira ya dhati ya Serikali katika kujenga Taifa lenye uchumi imara na ustawi wa wananchi kwa ujumla.

# PICHA ZA MIRADI  MBALIMBALI



Halmashauri  imefanikiwa kujenga shule maalumu ya awali na Msingi ya  mchepuo wa lugha ya kiingereza ambayo imejengwa kwa shilingi mil. 800 fedha za mapato ya ndani ambapo katika ziara yake Rais  Dkt. Samia Suluhu Hassani mnamo tarehe 24/09/2024 alipotembelea Mkoani Ruvuma alifanikiwa kufungua .







Katika kiPindi cha miaka (5) hali ya utoaji wa huduma ya maji imeimarika kutokea asilimia 82 hadi asilimia 92 katika Manispaa ya Songea, Manispaa ya Songea inatoa shukrani kwa Mheshimiwa Rais kwa mradi wa maji wa Bil 145.7 wa miji 28 katika Manispaa ya Songea ambapo mradi huo ukikamilika hali ya upatikanaji wa maji Manispaa ya Songea utakuwa asilimia 100.

Sekta ya miundombinu ya barabara Manispaa ya Songea imepokea kiasi cha Bil. 22 kwa ajili ya ujenzi wa barabara (TACTIC) za lami nzito katika kata za mjini yenye urefu wa KM 10.1 ambapo utekelezaji wake umefikia 89%.



Standi ya kuu ya Mabasi Songea ambayo imejengwa kwa kiasi cha Bil. 6.5.



Aidha, Mafanikio katika Sekta ya huduma za jamii (TASAF), Manispaa ya Songea jumla ya Bil.9 zimepokelewa na kulipwa kwa wafaidika 2514.

Asilimia 60 ya wakazi wa Manispaa ya Songea wamefaidika na ruzuku ya mbolea hivyo imewezesha kuimarisha uchumi wa kaya na wa Taifa ambapo katika kipindi cha miaka minne TAN 88,208 zimetolewa ruzuku kwa wananchi wa Manispaa ya Songea.
Aidha, Hali ya utoaji wa ikopo ya makundi maalumu wanawake 4%, vijana 4% na watu wenye ulemavu 2% katika kipindi cha miaka (4) Manispaa ya Songea imetoa jumla ya bil. 2,205,429,441 .

Hata hivyo, hivi karibuni Halmashauri imepata kibali cha kutoa mikopo kupitia benki ya NMB ambapo jumla ya Bil. 1.3 zipo katika hatua ya kukopeshwa.

Halmashauri imefanikiwa kulipa fidia ya jumla ya 5,300,000,000 kwa eneo la EPZA kata ya Mwenge Mshindo na shilingi Bilion 1.9 Bonde la Ruhira.

Ukusanyaji wa mapato ya ndani yameongezeka kutoka shilingi Bil. 2.1 hadi shilingi bil. 7.2 ambapo bajeti ijayo 2025/2026 Halmashauri inatarajia kukusanya jumla ya shilingi Bil. 9.1

.




Milioni 134,400,000  za jenga  madarasa  5 na matundu 8 ya vyoo fedha kutoka  Serikali kuu katika shule ya Sekondari  Matogoro ambapo ujenzi  umekamilika na umeanza kutumika.

# MIL. 521 KUJENGA  SHULE MPYA YA RUHUWIKO SEKONDARI




Shule mpya ya Sekondari Ruhuwiko inajengwa  kwa gharama ya mil. **521** fedha za SEQUIP ambapo mradi huo umeanza kutumika.

# UJENZI WA MADARASA 4 NA MATUNDU 8 YA VYOO SHULE YA SEKONDARI BOMBAMBILI





Mradi wa madarasa  4 na matundu 8 ya vyoo katika shule ya Sekondari Bombambili umejengwa kwa gharama ya shilingi  Milioni   110,400,000.00  fedha kutoka Serikali kuu mradi huo umekamilika na umeanza kutumika.

# MIL. 499 ZAJENGA SHULE MPYA YA DR DAMAS NDUMBARO





Ujenzi wa Vyumba vya madarasa 4 vimekamilika na vimeanza kutumika katika shule mpya ya Dkt. Ndumbaro iliyojengwa kwa shilingi 499,049,131.00 fedha za SEQUIP.

## MIL. 278.4 KUTOKA SERIKALI KUU ZAJENGA MADARASA 11 NA MATUNDU 8 YA VYOO SHULE YA SEKONDARI RUVUMA




Milioni 248,400,000.00 imetolewa na Serikali kuu kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 11 vya madarasa na matundu 8 ya vyoo shule ya Sekondari Ruvuma ambapo mradi huo umekamilika.

## MUONEKANO WA MADARASA MAPYA SHULE YA SEKONDARI LAWRANCE GAMA





# BIL. 1. 6 KUJENGA SHULE MPYA YA AMALI RUVUMA




Ujenzi wa madarasa, maktaba, na chumba cha kompyuta, bweni, maabara, nyumba ya mwalimu na bwalo la chakula ambapo ujenzi huo umegharimu shilingi Bil. 1,600,000,000 SEQUIP ambao upo katika hatua ya kupaua na kazi inaendelea.

## UJENZI WA VYUMBA 3 VYA MADARASA NA VYOO MATUNDU 8 SHULE YA SEKONDARI LUKALA



ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa umekamilika, pamoja na matundu 8 ya vyoo ambapo mradi huo umegharimu kiasi cha shilingi 86,400,000.00 fedha kutoka Serikali kuu.

# MIL. 180  UJENZI WA NYUMBA YA MKURUGENZI





Mil 180,000,000 zimetolewa na Serikali kuu kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea ambayo ipo hatua ya kuezekwa.

## ZAIDI YA BIL.22 ZAJENGA BARABARA ZA LAMI NZITO KM 10.1 KWA KATA YA MFARANYAKI, MJINI NA MAJENGO






Mradi wa Barabara umegharimu kiasi cha Bilioni 22,494,855,000.00 (TACTIC) ambao uko katika hatua za ukamilishaji.

## MIL.80 ZATUMIKA KUJENGA BWENI LA KITUO CHA WATOTO WENYE MAHITAJI (USONJI) SHULE YA MSINGI SUBIRA.





Bweni la Kituo cha shule ya Msingi Ruhila limejengwa kwa thamani ya Mil. 80,000 na Uzio jumla ya Mil. 60 ambacho kimeanza kutumika na kina jumla ya watoto wenye mahitaji maalumu 50 wakiwemo Wasichana 26 na wavulana 24.

## TAN 118,000 ZA MAHAINDI  ZANUNULIWA  KWA WAKULIMA KWA MWAKA 2024/2025

Wakala kanda ya Songea imefanikiwa kununua Tan 18,000 za mahindi zenye thamani ya Mil. 118,292,056 huku  mbaazi zikinunuliwa Tan  875 zenye thamani ya Mil.  82,804,439.820.




Akizungumza afisa manunuzi kanda ya Songea Endrew J. Massawe  alianza kwa kuipongeza Serikali kwa kuweza kufanikiwa kulipa madeni yote ya wakulima, “alisema”

## UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA 26, SHULE SHIKIZI NA BWENI S/M RUHILA – MAHITAJI MAALMU. 2020/2021

Halmashauri ya Manispaa ya Songea ilipokea fedha za mpango wa maendeleo ya Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO 19 ambazo ni kiasi cha Milioni 660,000,000.

Fedha hizo zilitolewa kutoka Serikali kuu chini ya uongozi wa Mheshiwa Rais wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa lengo la kutekeleza miradi ya maendeleo ndani ya Manispaa ya Songea.

Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa vyumba 26 vya madarasa katika shule za Sekondari kiasi cha shilingi 520,000,000,

Ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa katika shule ya msingi Nonga nonga kiasi cha shilingi 60,000,000, ujenzi wa bweni moja la wanafunzi katika shule ya msingi Ruhila yenye wanafunzi wenye mahitaji maalumu kiasi cha shilingi 80,000,000.

# **VYUMBA 26 VYA** MADARASA (UVIKO 19)









Ukamilishaji na ujenzi wa matundu 62 ya vyoo kwenye shule 13 za Msingi kwa gharama ya shilingi Mil. 69,492,000.00 fedha kutoka Serikali kuu kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ambapo miradi imekamilika na inatumika.



# HALI YA UTOAJI WA MIKOPO KATIKA KIPINDI CHA MWAKA 2020/2021

Halmashauri ya Manispaa imetenga eneo la ardhi yenye ukubwa wa ekari 15 iliyopimwa kwaajili ya kuvikopesha vikundi vya miradi mikakati ya viwanda vya kati na vidogo vya wanawake,Vijana na watuwenye ulemavu lilo mtaa wa viwandani kata ya Lilambo Manispaa ya Songea Kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Halmashauri imefanikiwa kuboresha huduma za mikopo yenye tija ya miradi ya viwanda kwa vikundi vya wanawake,Vijana na watu wenye ulemavu katika kutoa mikopo mikubwa yenye tija.

Idadi ya mikopo iliyotolewa ni pamoja na  vikundi vya Wanawake vikundi 64 Tsh 129,727,777.91, Vijana Vikundi  29  Tshs 64,267,777.91 na Watu Wenye Ulemavu Vikundi 8 Tshs 23,733,886 ikiwa na jumla ya fedha za mikopo zote Tsh 217,729,441.82 na kupelekea jumla ya vikundi 101.





Mil. 733,500,000 zatumika kujenga madarasa 30 na matundu ya vyoo 99 kwa shule za Msingi 18 Manispaa ya Songea katika mwaka wa fedha 2020/2021 (FEDHA ZA NJE ).



PICHA ZA MADARASA MBALIMBALI.

## UKAMILISHAJI WA KITUO CHA AFYA CHA RUVUMA.

Manispaa ya Songea katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021,

Ilipokea kiasi cha fedha Tsh Mil. 40,000,000 fedha kutoka Serikali kuu kwa ajili ya ukamilishaji Wa kituo cha afya Ruvuma ambapo mradi huo umekamilika na unatumika.



**Kituo cha afya Ruvuma**

# MIL. 500 FEDHA ZA TOZO ZILIVYOJENGA KITUO CHA AFYA MSAMALA.






Ujenzi umekamilka huduma zimeanza kutolewa

## MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

Halmashauri ya Manispaa ya Songea katika kipindi cha mwaka wa Fedha 2021/2022 ilipokea kiasi cha shilingi Mil. 112,500,000.00 kwa ajili ya Ukamilishaji wa vyumba vya madarasa 9 kwenye shule za Msingi 6 ambapo miradi hiyo imekamilika na inatumika.



Ujenzi wa Bweni la watoto wenye mahitaji maalum Shule ya Msingi Subira



Halmashauri ya Manispaa ya Songea imepokea Mil. 80 kwa ajili ya ujenzi wa bweni la watoto wenye mahitaji maalum Shule ya Msingi Subira, jengo limekamilika na linatumika

Halmashauri ya Manispaa ya Songea ilipokea kiasi cha shilingi Mil. 180,000,000 kwa ajili ya Ukamilishaji wa vyumba 12 vya maabara kwenye shule 6 za Sekondari ambapo miradi imekamilika na inatumika.



# MUONEKANO WA HOSPTALI YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA.




# KITUO CHA AFYA SUBIRA CHA JENGWA KWA MIL. 500 FEDHA ZA TOZO



Ujenzi umekamilika huduma zinaendelea kutolewa

## BIL. 1.2 ZATOLEWA MKOPO KWA WANAVIKUNDI WANAWAKE, VIJANA, NA WATU WENYE ULEMAVU KATIKA KIPINDI CHA MIAKA FEDHA 2020/2023

Halmashauri ya Manispaa ya Songea inaendelea kutoa mikopo ya asilimia kumi kwa vikundi vya wananwake 4%, vijana 4%, na watu wenye ulemavu 2% sawa na asilimia 10% katika kipindi cha miaka mitatu 3 kuanzia 2020 hadi 2023 Halmashauri hiyo imetoa jumla ya kiasi cha Tsh Bil. 1.2 kwa wanavikundi 133 wenye wanachama 661.

Lengo kuu la mikopo hiyo ni kukuza ajira kwa wanakikundi na kuongeza kipato kwa jamii.





**MIKOPO YA VIKUNDI ILIYOTOLEWA KWA WANAWAKE 4%,VIJANA 4% NA WATU WENYE ULEMAVU 2% KATIKA KIPINDI CHA 2021/2022**

Halmashauri ya Manispaa ya Songea, imetoa mikopo kwa vikundi vya wanawake 9 Tshs 420,000,000 Vijana vikundi 5 Tshs 179,000,000.00 na Watu Wenye Ulemavu 2 Tshs 20,000,000 vikundi ikiwa na jumla ya Tsh 619,000,000 na kupelekea jumla ya vikundi 16.



KIKUNDI CHA AMANI KATA YA MISUFINI.
WAUZAJI WA MAFUTA YA ALIZETI


KIKUNDI CHA TUIKE KATA YA LIZABONI.
UFUGAJI WA NGURUWE.

# HALI YA UTOAJI WA MIKOPO YA VIKUNDI VYA WANAWAKE 4%,VIJANA 4% NA WATU WENYE ULEMAVU 2% KATIKA KIPINDI CHA 2021/2022






# PICHA MBALIMBALI ZA KITUO CHA AFYA LILAMBO.



Mil. 50,000,000 ilitolewa kwa ajili ya ukamilishaji wa Zahanati ya Makambi fedha kutoka Serikali kuu ambapo mradi umekamilika na umeanza kutumika.



## MIKOPO KWA VIKUNDI KATIKA KIPINDI CHA MWAKA 2022/2023

Utoaji wa mikopo kwa vikundi vya wanawake 3 Tsh 35,000,000, vikundi vya Vijana 10 Tshs 311,700,000 na Watu Wenye Ulemavu kikundi 3 Tshs 22,000,000 na kupelekea jumla ya Tsh 368,700,000 kwa vikundi 16.



KIKUNDI CHA USHONAJI – WANAWAKE 4%

Halmashauri ya Manispaa ya Songea ilipokea fedha kiasi cha shilingi Mil. 55 kwa ajili ya Ujenzi wa vyumba vya madarasa 2 na matundu ya Vyoo 6 na vifaa vya michezo darasa la awali shule ya Msingi Mbulani.






# BIL. 1.52 ZATATUA CHANGAMOTO YA MADARASA SONGEA MC

Halmashauri ya Manispaa ya Songea Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ilipokea jumla ya kiasi cha **shilingi 1,520, 000,000.00 kutoka serikali kuu** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta ya Elimu ambapo jumla ya madarasa 76 yamejengwa katika shule za sekondari 19 na hivyo kukidhi mahitaji ya kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza katika mwaka wa masomo 2023.

Aidha, Mradi huo ulianza kujengwa tarehe 14 oktoba 2022 na kukamilika tarehe 12 Desemba 2023 na umeanza kutumika ambao umewezesha kupokea jumla ya wanafunzi 3,800 wa kidato cha kwanza mwaka 2023

.



# PICHA ZA MIRADI YA MADARASA 76, VITI NA MEZA 3,800




MSAMALA SEKONDARI
UJENZI WA VYUMBA 11 VYA MADARASA
MIL.220,000,000


BOMBAMBILI SEKONDARI
UJENZI WA VYUMBA 7 VYA MADARASA
MILIONI 140,000,000


MATOGORO SEKONDARI
UJENZI WA VYUMBA 2 VYA MADARASA
MILIONI 40,000,000




LONDONI SEKONDARI
UJENZI WA VYUMBA 6 VYA MADARASA
MILIONI 120,000,000


Songea MC
Ujenzi wa Kituo cha Maegesho ya Malori Kata ya Lilambo




KALEMBO SEKONDARI
UJENZI WA VYUMBA 2 VYA MADARASA
MILIONI 40,000,000




LIZABON SEKONDARI
UJENZI WA VYUMBA 6 VYA MADARASA
MILIONI 120,000,000


LUWAWASI SEKONDARI
UJENZI WA VYUMBA 6 VYA MADARASA
MIL.120,000,000




LUKALA SEKANDARI
UJENZI WA VYUMBA 4 VYA MADARASA
MIL.80,000,000


CHANDARUA SEKONDARI
UJENZI WA VYUMBA 6 VYA MADARASA
MIL.120,000,000


SILI SEKONDARI
UJENZI WA VYUMBA 3 VYA MADARASA
MIL.60,000,000


ZIMANIMOTO SEKONDARI
UJENZI WA VYUMBA 5 VYA MADARASA
MIL.100,000,000


MLETELE SEKONDARI
UJENZI WA VYUMBA 4 VYA MADARASA
MIL.80,000,000

Halmashauri ya Manispaa ya Songea katika Kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 ilipokea kiasi cha Tsh Mil. 100 kutoka Serikali kuu kwa ajili ya Ujenzi wa chumba cha ICT na maktaba shule ya sekondari Luhira ambapo mradi huo hatua ya ukamilishwaji.

Mil. 540,000,000 za kamilisha Ujenzi wa vyumba vya madarasa 7 na mabweni 4 kwenye shule za sekondari Emmanuel Nchimbi.



MAKTABA LUHIRA SEKONDARI



MABWENI 4 YA SHULE YA SEKONDARI Emmanuel Nchimbi

# MUONEKANO WA SHULE YA SEKONDARI  EMMANUEL NCHIMBI






# MUONEKANO WA MADARASA SHULE YA SEKONDARI RUHILA (SHULE MPYA)





Ukamilishaji wa vyumba vya madarasa 12 kwenye shule za Msingi 7 kwa gharama ya Mil. 156,250,000 katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 katika Shule ya Msingi Chief Mbano.





SHULE YA MSINGI KIPERA

# MIL. 545 ZA JENGA KITUO CHA AFYA MLETELE ( FEDHA ZA NJE)

Wananchi wa kata ya Mletele wanatoa shukrani kwa Serikali ya awamu ya Sita inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuwajengea kituo cha afya cha kata ya Mletele ambacho kimewezesha kupunguza kero ya umbali wa upatikanaji wa huduma za Afya zitolewazo katika ngazi ya kituo cha Afya.

Ujenzi wa kituo cha afya Mletele umegharimu kiasi cha Shilingi Mil. 545,857,968.26 fedha kutoka ufadhili wa Global Fund ambao ulianza kujengwa tarehe 17 juni 2022 ambao umeanza kutoa huduma za awali za matibabu ya wagonjwa wa nje (OPD).

Manufaa ya mradi huo kwa wananchi watakuwa wamepunguziwa msongomano kwa wagonjwa katika kituo cha Afya Mjimwema na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa pamoja na kupunguziwa umbali wa kufuata huduma za afya.



# MIL. 20 FEDHA ZA MAPATO YA NDANI  ZINAVYOTATUA CHANGAMOTO  ZA  KATA 21.

Halmashauri ya Manispaa ya Songea imekuwa ikiendeleza historia ya kutoa fedha Mil. 20 kila kata kwa kila mwaka ili kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili kata husika.

Aidha kwa mwaka 2022/2023 Manispaa ya Songea imetoa fedha Mil 20 ambazo zimefanya kazi za kutekeleza shughuli mbalimbali za miradi ya maendeleo za kata ikiwemo na utengenezaji wa kivuko  cha Mtaa Mtaungana kuelekea kata ya Mjimwema, uchongaji  na ufunguzi wa  wa barabara za mitaa Miembeni, Merikebu na Mtakuja kata ya Bombambili.

Miradi mingine iliyotekelezwa kupitia mgao wa fedha Mil 20 fedha za mapato ya ndani ni pamoja na Ujenzi wa Ofisi ya Lami kata ya Subira, Umaliziaji wa bweni la shule ya Mdandamo Sekondari na miradi mingineyo.

# MIL. 20 FEDHA ZA MAPATO YA NDANI  ZINAVYOTATUA CHANGAMOTO  ZA KATA




Ofisi ya Mtaa wa Lami



Kivuko cha Mtaa wa Mtaungana - Msamala



Umaliziaji wa Bweni



Umaliziaji wa ofisi ya mtaa mang’ua.

**HALI YA UTOAJI WA MIKOPO KWENYE VIKUNDI KATIKA KIPINDI CHA MWAKA 2022/2023**




Eneo la viwanda kwa wajasiliamali Wanawake, Vijana na Walemavu kupitia 10% za Mapato ya ndani.



**KIKUNDI CHA USELEMALA- (VIJANA) 4%**



KIKUNDI CHA KUKAMUA MAFUTA YA ALIZETI- (WANAWAKE) 4%

## MIKOPO YA 10% INAVYOINUA KIPATO KWA VIKUNDI VYA VIJANA, 2022/2023

## ( **KIWANDA CHA** VIFUNGASHIO)









Mil 560,000,000 zajenga shule ya sekondari ya Lawrance Gama katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024 hadi machi fedha kutoka kwa Wafadhili ambapo ujenzi umekamilika na umeanza kutumika







Ujenzi wa vyumba vya  madarasa 10  sekondari  ya Londoni kwa  Shilingi 242,500,000.00  fedha kutoka Serikali kuu mabapo mradi  huo umekamilika.






Songea MC
Barabara za Mitaa Kata ya Msamala

# Muonekano wa Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Ruvuma



KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI MANISPAA YA SONGEA.

TOVUTI; www.songeamc.go.tz

SONGEA ONLINE TV

songea MC

Songea MC

Songea MC

*Kazi na Utu Tunasonga mbele.*